PRIMARY END TERM 3 EXAMS
2016

KISWAHILI
STD 5

,
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

DARASA LA TANO

KISWAHILI

MUDA: SAA1 DAKIKA40

Soma kifungu vifuatavyo kisha ujaze nafasi zilizoachwa kuanzia 1 - 15.

Utajiri ____1____ Omari ulijulikana kote nchini. Kujionyesha ____2____ kulitambuliwa ____3____ wengi. Hakuna kilichokosekana nyumbani ____4____. Mkewe ____5____ hatoki ____6____ sonara. Mara anafua mikufu, mara vikuku, mara bangili ____7____ herini. Lakini ____8____ vilikuwa ni kazi ____9____. Mkewe alizidi kukonda ____10____ kukondeana. Jambo ____11____ liliwastaajabisha majirani ____12____. Jirani yao ____13____ aliyeitwa Ali alimtembelea Omari ____14____ ushauri. Alimshauri kumpa bibi yake nyama ya ulimi ____15____ siku.

1.	A. ya	B. wa	C. la	D. za
2.	A. mwake	B. chake	C. kwake	D. vyake
3.	A. na	B. ya	C. pa	D. si
4.	A. wake	B. mote	C. lote	D. kwake
5.	A. alikua	B. alikuwa	C. hakua	D. wakawa
6.	A. kua	B. hata	C. kwa	D. ili
7.	A. hawa	B. sana	C. kama	D. au
8.	A. vyote	B. yote	C. zote	D. wote
9.	A. vizuri	B. mazuri	C. bure	D. tena
10.	A. na	B. sasa	C. wala	D. ila
11.	A. hii	B. hili	C. hizi	D. huu
12.	A. hadi	B. kama	C. sote	D. sana
13.	A. kizuri	B. nzuri	C. mzuri	D. wazuri
14.	A. kukipa	B. kulimpa	C. kuzipa	D. kumpa
15.	A. mara	B. kila	C. nyingi	D. hata

Kutoka swali la 16 - 30, jibu kila swali kulingana na maagizo

16. *Kanusha sentensi:* Amina ameenda sokoni.
A. Amina hataenda sokoni
B. Amina hakuenda sokoni
C. Amina hajaenda sokoni
D. Amina amerudi kutoka sokoni

17. Andika kwa wingi: Mti ule utakatwa kesho.
A. Miti yale yatakatwa kesho
B. Miti zile zitakatwa kesho
C. Miti ile zitakatwa kesho
D. Miti ile itakatwa kesho

18. Kinyume cha neno kijana ni
A. mzee B. msichana
C. mwanamke D. mvulana

19. Umbo hili ni gani?

A. Pia
B. Mstatili
C. Mraba
D. Duara dufu

20. Makao ya kuku ni
A. mzinga
B. kombe
C. kizimba
D. kasri

21. Neno 'kipepeo' liko katika ngeli gani?
A. A - WA
B. KI - VI
C. I - ZI
D. LI - YA

22. Kamilisha sentensi: Mbuzi _____ watachinjwa kesho.
A. zile
B. yule
C. vile
D. wale

23. Kamilisha methali: Mvumilivu hula
A. mbichi
B. mbivu
C. yote
D. chakula

24. Chagua nomino katika sentensi
Yule ni nyoka mkubwa.
A. ni
B. yule
C. mkubwa
D. nyoka

25. Mtoto wa ng'ombe ni
A. ndama
B. kinda
C. shi[illegible]
D. kifaranga

26. Shairi la mishororo minne katika kila ubeti huitwa
A. tathlitha
B. tarbia
C. takhmisa
D. thumni

27. Akisami hii huitwaje, $\frac{1}{5}$?
A. humusi
B. robo
C. thuluthi
D. thumni

28. Chagua neno ambalo halifai katika orodha ifuatayo:
A. Punda
B. Ng'ombe
C. Simba
D. Kondoo

29. Tegua kitendawili: Popote niendapo hunifuata
A. kifuli
B. shoka
C. kisogo
D. kivuli

30. Kaka yake mama huitwaje?
A. Ami
B. Shangazi
C. Mpwa
D. Mjomba

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40

Katika kijiji cha Maliwaza, paliishi mzee mmoja aliyejaliwa kuwa na watoto watano wa kiume. Mzee Salim, jinsi alivyojulikana alikuwa tajiri sana. Kando na kuwa na mali nyingi, mzee Salim pia alikuwa na hekima. Mara nyingi watu walikuwa wakienda kwake kupata ushauri. Vijana wake walijifunza kufanya mambo tofauti tofauti. Waliokuwa wakubwa walitekeleza majukumu tofauti tofauti. Kitinda mimba naye aliaminiwa jukumu la kutunza mifugo yote ya babaye.

Ulifika wakati ambapo mzee Salim aliona kwamba ni kama maisha yake yamefika upeo wa kuendelea. Alikata shauri kuwaita wanawe ili awape urithi wake pamoja na usia wake. Wote walifika upesi pale ili wasipitiwe na lolote licha ya shughuli zao nyingi mno na kutafuta riziki zao.

Walipokusanyika pale mzee hakuchelea kutekeleza lililomfanya kuwaita wanawe. Alifahamu kuwa kidogo tu angeaga dunia. Hivyo basi akaanza kutoa usia wake na kisha kuwapa urithi wao.

31. Mzee Salim alikuwa na watoto
A. sita
B. wanne
C. wawili
D. watano

32. Watoto wote wa mzee Salim walikuwa
A. wasichana
B. wavulana
C. wa kike
D. wanawake

33. Kinyume cha neno tajiri ni
A. maskini
B. mzima
C. dhaifu
D. mgonjwa

34. Watu walikuwa wakienda kwa mzee Salim kupata
A. mali
B. chakula
C. zawadi
D. ushauri

35. Aliyepatiwa jukumu la kutunza mifugo ni
A. kifungua mimba
B. kitinda mimba
C. mtoto wa pili
D. Salim mwenyewe

36. Mzee Salim alikuwa na
A. hekima B. uzembe
C. hasira D. madharau

37. Mzee Salim alipowaita wanawe, alitaka kuwapa
A. urithi B. kazi
C. wake D. watoto

38. Maana ya urithi ni
A. maneno ya kutia nguvu
B. sheria za kinyumbani
C. ugonjwa wa kuambukiza
D. mali anayoachiwa mtu na wazazi baada ya kuaga

39. Vijana waliofika kwa babao walipoitwa walikuwa
A. sita
B. watano
C. watatu
D. wanne

40. Maana ya msemo 'angeaga dunia' ni
A. angetoroka
B. angehamia kwingine
C. angefariki
D. angetafuta mali

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali41 -50

Mwaka wangu wa tano shuleni, nilichaguliwa mbele ya walimu na wanafunzi wenzangu kuwa kiraja mkuu wa shule. Kura iliikuwa ni bayana. Waliopendekezwa majina yao kugombea uongozi walipiga foleni uwanjani kisha wanafunzi wakaruhusiwa kusimama nyuma ya yeyote yule wangempenda awe kiranja wao.

Mlolongo wa vijana waliokimbia nyuma yangu kuniunga mkono haungemithilika. Nilishinda kwa kiwango kikubwa sana. Naam, chanda chema huvikwa pete na mcheza kwao hutunzwa. Tuzo niliyopewa ni kuchaguliwa mbele ya wenzangu kwa nderemo na shangwe.

Maendeleo yangu yalikuwa mema. Nililaani kushika nambari chini ya tatu. Lazima ningekuwa kielelezo kwa wengine. Niliikuwa na bidii na nia ya kufanya vizuri shuleni. Na penye nia pana njia. Huo ndio ulikuwa wito wangu kila wakati.

41. Mwandishi alichaguliwa kuwa kiranja wa shule mwaka wake wa ngapi shuleni?
A. Sita
B. Tatu
C. Nne
D. Tano

42. Mwandishi alichaguliwa kuwa kiongozi wa
A. walimu
B. wanafunzi
C. wazazi
D. wabunge

43. Maana ya neno 'bayana' ni
A. wazi
B. kelele
C. fujo
D. pekee

44. Foleni iliipigwa wapi?
A. Darasani
B. Ofisini
C. Uwanjani
D. Msituni

45. Wanafunzi waliomuunga mkono mwandishi walikuwa
A. wachache
B. wawili
C. wanane
D. wengi

46. Ni kweli kuwa mwandishi alikuwa
A. mwerevu
B. mjinga
C. mfupi
D. maskini

47. Kati ya methali zilizotumiwa katika kifungu ni ipi inayotuhimiza kuwa tukiwa na moyo wa kufanya jambo tutafanikiwa?
A. Mcheza kwao hutunzwa
B. Penye ni pana njia
C. Haraka haraka haina baraka
D. Asiyekubali kushindwa si mshindani

48. Tuzo ni
A. Adhabu
B. chanda
C. zawadi
D. hasara

49. Ni jambo gani ambalo mwandishi hakulifurahia?
A. Kuchaguliwa kiranja mkuu
B. Kutenda wema
C. Kuchaguliwa na vijana wengi
D. Kushika nambari chini ya tatu

50. Kichwa kinachofaa habari hii ni
A. Uchaguzi wa wabunge
B. Kutia bidii shuleni
C. Uchaguzi wa kiranja mkuu
D. Siku ya sherehe shuleni